

Sumu ya risasi inaweza Kuzuiwa kwa asilimia 100



Osha mikono ya mtoto wako kabla ya kula, vitafunio na kulala.



Rekebisha rangi inayochipuka au kuambua.



Osha wanasesere, chupa na matiti bandia mara kwa mara.



Osha kwa maji na upanguze kwa maji maeneo ya kuchezea.



Kula chakula chenye kiasi kikubwa cha madini, kalisi na Vitamini C.



Epuka peremende, wanasesere, vipodozi na suluhu za nyumbani zilizoingizwa kutoka nchi za nje.



Tumia maji baridi ya mfereji kupika kutayarisha chupa au kunywa.



Linda Watoto Wako Dhidi ya Sumu ya Risasi



Health and
Human Services

Public Health

Tembelea ukurasa wa Childhood Lead Poisoning Prevention Program katika hhs.iowa.gov au piga simu 1-800-972-2026 ili upate maelezo zaidi kuhusu kuzuia sumu ya risasi kwa watoto.



Health and
Human Services

Public Health

Ni Nini Kinachosababisha Sumu ya Risasi?



Huenda watoto wakawa katika hatari ya risasi ikiwa wanaishi au kutembelea nyumba zilizojengwa kabla ya 1978. Vyanzo vingine vya risasi vinaweza kuwa:

- ▶ Ya Kale
- ▶ Glasi yenye waa
- ▶ Marekebisho ya nyumbani
- ▶ Funguo
- ▶ Vyambo vya kuvua
- ▶ Peremende zilizoingizwa kutoka nchi za nje
- ▶ Marekebisho ya magari
- ▶ Viungo



Funguo za shaba nyeupe



Vyombo vya udongo wa kiufundi



Rangi ya risasi kwenye madirisha ya zamani



Ya Kale

Ishara za Sumu ya Risasi ni Zipi?



Huenda watoto wengi walio na sumu ya risasi wasionekane wagonjwa, lakini huenda baadhi ya ushara zikajumuisha:

- ▶ Anasisimka kwa urahisi
- ▶ Kuudhika
- ▶ Anatatizika kuwa makini
- ▶ Ugumu wa kujifunza
- ▶ Matatizo ya tumbo na kutapika
- ▶ Kupungua kwa uzito
- ▶ Ukuaji kwa kasi ya chini
- ▶ Kuumwa na kichwa
- ▶ Kuchelewa katika ukuaji
- ▶ Uchovu kupita kiasi



Inapendekezwa watoto wote wapimwe wakiwa na umri wa miezi 12 na 24 na wanapaswa kutathminiwa iwapo wako katika hatari kila wakati wanapotembelea hospitali.

Vipimo vya risasi kwenye damu hufanya kazi vipi?

Kuna aina mbili za vipimo vya risasi kwenye damu: kapilari na damu ya vena. Kipimo cha **kapilari** hutumia kiasi kidogo cha damu kutoka kwenye kidole ili kuangalia uwepo wa risasi, matokeo yanapatikana ndani ya dakika kadhaa. Kipimo cha kapilari kikionyesha uwepo wa risasi, kipimo cha damu ya **vena**, iliyotolewa kwenye mkono, itadhibitisha viwango vya risasi kwenye damu.

Kiwango cha Risasi Kwenye Damu ya Mtoto Wako

_____ ana kiwango cha risasi kwenye damu cha mikrogramu _____ kwa kila desilita ($\mu\text{g}/\text{dL}$)

Kwa Kiwango cha Risasi kwenye Damu cha chini ya $3.5 \mu\text{g}/\text{dL}$, huhitaji kufanya chochote. Endelea kuwa na ufahamu wa uwezekano wa kuathiriwa na hatari za risasi kwenye mazingira.

Kwa Kiwango cha Risasi kwenye Damu cha Kati ya $3.5-9 \mu\text{g}/\text{dL}$, muulize mtoa huduma wako kuhusu kutambua vyanzo vya risasi na umuhimu wa lishe bora na utunzaji wa nyumba.

Kwa Kiwango cha Risasi kwenye Damu cha $10 \mu\text{g}/\text{dL}$ au zaidi, mtoto wako anahitaji ufuatiliaji wa ziada. Angalia hapa chini ili upate muda sahihi wa kufanyiwa kipimo tena.

Matokeo ya Mtoto Wako

Matokeo	Tarehe ya Kipimo cha Damu ya Vena
10-14	Ndani ya miezi 3
15-19	Ndani ya mwezi 1
20-44	Ndani ya wiki 1
45-69	Ndani ya saa 48
70 au zaidi	MARA MOJA

Mtoto wako anapaswa kufanyiwa kipimo kufikia tarehe hii:
